Zawadi ndogo kwako

Usikate tamaa! Stahimili!



Gabriele

Usikate tamaa!
Stahimili!

Maandishi ya Gabrieli, nabii na mjumbe wa Mungu kwa wakati wetu

First Edition in Swahili: July 2019

1ère édition en Swahili: juillet 2019

Translated from the original German title:
Traduit de l'allemand, titre original:

Lass nicht los! *(g328sw)*

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents

Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés

Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Usikate tamaa ! Stahimili !

Watu wengi wanakuwa kama wenye kuchanganyikiwa wanaposikia neno « MUNGU ». Ujumbe huu « Usikate tumaini, vumilia ! », hauna uhusiano na mungu wa makanisa ya kishirika, na mungu huyo anayedhaniwa kwamba anaishi katika vitu vilivyochorwa vizuri, mungu ambaye eti ana haja ya waombezi ambao wana wajibu wa kumfikishia mahitaji ya watu, kufuatana na dhana zinazotokana na mpango wa daraja za utakatifu katika kanisa. Kuamini hayo ni kufuata kama kipofu viongozi ambao nao ni vipofu, kwa sababu mafundisho ya Yesu wa Nazareti ina ujumbe tofauti kabisa na ule. Ujumbe huo unatuambia kwamba mafundisho yote ya Yesu yana maana.

Alitutolea sala ya « Baba yetu » na akatufundisha kwamba katika sala tunaweza kusimulia na Mungu, Babaye na Baba yetu. Kupitia sala ya « Baba yetu », Yesu wa Nazareti alitufundisha kumjua vema Mungu, Baba yetu wa

mbinguni, ambaye tunaweza na tunapashwa kugeukia moja kwa moja katika maombi, bila mpatanishi wa kieklezia. Kwa upekee sala ya « Baba yetu » inajaa mafundisho kwa wale walio na fikra safi, endapo mtu anaamini kuwepo kwa Akili ya juu sana yaani Mungu na ikiwa sala hiyo ya Baba Yetu haitamkwi kama maneno matupu tu yanayonenwa kimoyomoyo, bila heshima kuu kwa Mmoja wa Ulimwenguni pote.

Mungu, Baba yetu sisi sote, hakuongoza watu katika nyumba ya mawe, kwani tangu kale kupitia nabii wake Isaya alisema: *« Mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia kikalio cha miguu yangu, nyumba gani mnaweza kunijengea ? »* Roho huru, Roho wa ukweli, haishi kamwe ndani ya makanisa iliyojengwa kwa mawe. Yesu, Kristo, alituarifu kwamba Mungu yumo ndani mwetu wakati aliposema kwamba mtu ni hekalu la Mungu na Mungu anakaa ndani ya mtu.

Shauri lake la kutualika tuingie katika chumba cha ndani kusudi ya kuomba kwa kimya,

Mungu, Baba yetu wa mbinguni, anayekaa ndani mwetu, inatupatia nguvu wakati wa shida, uchungu na dhiki, kwa sababu nguvu na msaada vinapatikana katika sala ya ukimya.
Yesu anasema: *« wakati unapotaka kuomba, ingia katika chumba chako cha ndani, funga mlango wako, omba Baba yako aliye hapo kwa siri, na Baba yako, anayeona kwa siri, atajibu maombi yako ».*

Anayetegemea mafundisho ya Yesu wa Nazarethi anaelewa maana ya maneno « Usikate tumaini, stahimili ! », ambayo ina maana pia ya kufuata mafundisho ya Yesu wa Nazarethi.

« Usikate tumaini, vumilia ! », ni sentensi ndogo inayosema na moyo wetu. Ina maana ya kina kwa watu wanaoamini nguvu kuu iliyo ndani mwetu na iliyo na uwezo wa kutuunga mkono na pia kututolea kwa wingi nguvu na msaada.

« Usikate tumaini, vumilia ! », ina maana: shikilia sana Roho huru wa upendo, Yule Anayeishi ndani mwako, ndani mwetu sisi sote.

« Usikate tumaini, stahimili ! » mtolee sala zako katika chumba chenye kimya. Mtolee sala zako katika nyakati ngumu, hasa wakati unapokumbwa na hali ya kukata tumaini.

« Usikate tamaa, stahimili ! » husaidia kupata utulivu wa ndani, ukimya na amani, ambavyo hutusaidia kutambua kuwepo kwa Mungu.

Usikate tumaini, stahimili ! Omba Mungu akusaidie kutoka katika fikra na hisia mbaya. Omba Mungu wakati unapokabiliwa na kukosa tumaini, na magonjwa na hata pia shida. Omba Mungu akusaidie kupata amani, uhuru na mafanikio. Usikate tumaini, stahimili !

Usikate tumaini, vumilia ! Omba Mungu ndani mwako akusaidie kutolea upya muelekeo mzuri hisia na mawazo yako, tabia yako yote. Omba Mungu akusaidie kuona na kuelewa mambo kwa kina, kuwa na mtazamo wa jumla, akusaidie kuwa huru na mwenye furaha.

Usikatetumaini,vumilia!Munguninuru,nanuru yake inataka kukufanya mwenye kungaa sana.

Usikate tamaa, stahimili ! Shikilia sana nguvu ya milele iliyo ndani mwako, kwa sababu wewe ni hekalu la Mungu na Mungu ndani mwako ni chemchem ya milele ya uzima wa milele.

Usikate tumaini, stahimili ! Baki na Mungu, hata kama unakabiliwa na mashaka dhidi Yake. Hata hivyo, mshikilie sana, kwa sababu anakupa nguvu na msaada. Usikate tumaini, stahimili, kwa sababu mwanga mdogo unatokea mahali fulani.

Usikate tumaini, stahimili ! Hata ukijihisi kwamba umetupiliwa na watu wote. Uwe na uhakika kwamba kuna Mmoja ambaye yupo pamoja nawe. Mmoja anayekujua, ambaye anapenda utu wako halisi. Kuna Mmoja anayekupa nguvu na ujasiri. Ni Roho wa Baba yako, wa Baba yetu wa mbinguni aliye ndani mwetu sote. Ndiyo sababu, Usikate tumaini, vumilia !

Usikate tumaini, vumilia ! Ndani ya nafsi ya kila mmoja wetu mna utajiri mkubwa unaotoa faida bila kukoma.

Usikate tumaini, stahimili ! Omba hata wakati sala zako ni za juu juu sana. Omba, Usikate tumaini, vumilia.

Usikate tumaini, vumilia ! Omba kusudi ugeuke mwema na msikivu kwa jirani yako. Omba kusudi upate mazuri ndani ya mabaya, kwani katika kila kitu, mna pande hizo mbili.

Usikate tumaini, vumilia ! Omba faraghani kwa ukimya, kwa sababu Yesu wa Nazareti alitufundisha kitu ambacho tungepashwa kukumbuka siku zote: *« Wakati unapotaka kuomba, ingia katika chumba chako cha ndani, funga mlango wako na mtolee sala Baba yako aliye katika siri. Na Baba yako anayeona katika siri atakujibu ».*

Usikate tumaini, vumilia, dumu katika kukuza wema na amani. Ila hayo haimaanishi kunyamaa mbele ya hatari iliyo dhahiri au hali isiyo ya uhaki au kufumbia macho dhuluma; lakini tuyajadilie kwa usikivu, ukarimu na uvumilivu, kwani Yule anayeona ndani, anajua ya kwamba katika mabaya mna mazuri pia. Ndiyo maana: Usikate tumaini, stahimili !

Baki kimya na utambue kwamba kabla ya kunena ni vema kuchunguza maneno ambayo unataka kutumia na kumuambia tu mwenzio yale ambayo kwa sasa ana uwezo wa kuyakubali. Ni mamoja pia kwa matendo yako.

« Usikate tumaini, vumilia ! » Ina maana tena, kutumia busara hususan katika mazungumzo na watu, kusudi tuweze kupata kwa pamoja suluhisho ya magumu, shida na matatizo yetu au ya jirani yetu. Ni faida kwa wote ikiwa tunamsaidia jirani yetu kupata suluhisho kwa magumu yake, akihitaji msaada huo.

Tungepashwa siku zote kujifunza kujitambua sisi wenyewe, kwa lengo la kuelewa taarifa ambayo mchana wetu unatutolea, na kuelewa kwamba ujumbe wote ambao mchana unatututolea una maana, kwani yote hutegemea kanuni ya « kutoa na kopokea ».

Mambo yote ya mchana ni ujumbe tunaotolewa, kwa sababu mchana huo ni wetu na kila mtu anaishi mchana wake mwenyewe. Tukitaka kufahamu jambo linalotuhusu katika

maneno tunayosikia na mambo tunayoishi, tunapashwa « kufungua barua » tunazotumiwa kila siku, yaani kufikiria juu ya maana ya ujumbe tunaopokea. Ndani ya kila ujumbe unaoletwa mna pia jibu na suluhisho, hata wakati, kwa mfano, watu wanazungumza nasi au tunaposikia yale yanayosemeka juu ya watu wengine.

Jambo linalotugusa wakati ule, hata lile linalotukasirisha na kututia hasira, lina ujumbe unaotaka kutuambia kitu fulani.

Kwa hiyo, tunarudilia: yaliyomo ndani ya kila hisia, kila wazo na kila neno, ni ujumbe unaotolewa. Hapa pana swali hili: ni nani basi anayepokea yale ambayo sisi au wengine tunayotoa ?
Kila mtu anapokea yale anayoyatoa; ni masafa yake, ni urefu wa mawimbi yake.

Ndiyo maana kila siku, tunapashwa kutafakari kuhusu yale tunayotoa, na kujiswali ni upi uzito wa hisia, mawazo na maneno yetu, na kwa nani tunavielekeza.

Tujiswali tena: kupitia hisia na mawazo ninayotoa, ni wazo au hisia gani ninalotaka kuongezea uzito kwa wengine na ni wazo na hisia gani watakayotoa baadaye, na ambayo nitapokea nami vilevile ? Kuona kwamba urefu wa mawimbi na masafa inayofanana hujikusanya pamoja, inawezekana kwamba mawazo na hisia zao ziturudilie na kutia nguvu hisia na mawazo yetu.

Turudilie swali hili: Ni upande wa mtu yupi tunaweza kutoa ujumbe na ni nani anayeupokea ? Kila mtu hupokea yale anayoyatoa, iliyo sawa na urefu wa mawimbi yake.
Hapa tunashauriwa hivi: fanya angalisho ! Kila siku ni siku yako. Ni nini unayotoa na ni nini unayopokea ?

Hakika, sisi wote tumekwisha kutambua kwamba kuna mawazo yanayojitokeza kwa ghafla ndani mwetu na yanayotuacha tujiswali: « mawazo haya yametokea wapi ? »
Lakini, badala ya kuichambua kwa ajili ya kupata jibu na suluhisho, mara nyingi tunaendelea kurudilia mawazo yanayofanana na hayo.

Yale yanayopitikana ndani ya hisia na fikra zetu, hutokana tu na sisi wenyewe. Ikiwa tabia yetu, programu au desturi zetu ni mbaya, tutapokea mambo mabaya inayoambatana na hayo. Lakini, ikiwa uwezo wetu wa kutoa ni mzuri, tutapokea basi mambo mazuri. Hayo hutokana kabisa na sisi wenyewe, ila si kutokana na yale ambayo jirani yetu huwaza au kutoa.
Ndio maana tunahimizwa: Usikate tumaini, vumilia !

« Usikate tumaini, vumilia ! », shauri hili linataka kutuhimiza tumgeukie Mungu, mtoaji wa milele, akili ya juu sana, nguvu tukufu iliyo ndani mwetu. Mungu, mtoaji wa milele, anajua kila jambo. Tupangilie maisha yetu tukimtegea kwa kuambatanisha siku zote fikra, maneno na matendo yetu na sheria ya Uzima.

Tunaweza kuchukua kwa mfano, kama vigezo, Amri za Mungu tulizotolewa kupitia Musa na Mafundisho ya Yesu wa Nazareti, hususan Mafundisho yake mlimani. Halafu tutatoa mambo mazuri na tutapokea pia mambo ma-

zuri, iliyo na msaada na suluhisho, kwa sababu Yule anayekaa ndani mwetu, Kristo wa Mungu, yupo daima pale kwa kutuhudumia na kutusaidia. Ndiyo sababu: Usikate tumaini, vumilia !

Usikate tumaini, stahimili katika shida zote, matatizo na mashaka yanayokupata.

Usikate tumaini, vumilia, hata kama leo unakumbwa na kukata tamaa, hata kama unachoka na kujihisi mwenye kutupiliwa na watu wote. Uwe na imani kwamba kuna Mmoja asiyekuacha kamwe, ni Mungu wa milele ndani mwako, ambaye ni upendo.
Ndiyo sababu: Usikate tumaini, vumilia ! Usikate tumaa, kwani nguvu halisi, nguvu ya Mungu imo ndani ya vyote. Mungu, Mtoaji mtukufu wa milele wa upendo, husaidia katika kila jambo. Ndiyo sababu: Usikate tumaini, vumilia !

Ingelitupasa mara na mara kufikiri ya kwamba kila kitu, hakika kila kitu hutegemea nguvu. Kwa hiyo tujiswali: kiwango changu cha

utoaji nguvu ni kipi ? Kwa sababu ni hayo ndiyo inaonyesha upeo wake.
Ingelitupasa mara tena kujiswali: « Ninatoa nini ? Ni nini watakaopokea wale ambao uwezo wangu wa kutoa unaweza kuwafikia ? » « Watu hao watatoa nini nao pia, na ni nini ambayo nitakayopokea baadaye nami ? »

Tufikirie juu ya jambo kwamba ujumbe mbaya unaotolewa na kila mmoja wetu siku baada ya siku haukosi madhara. Kwa wakati fulani, nguvu hizo zinaturudilia. Hayo yanaweza kutokeza sababu au tena mlolongo wa sababu na matokeo, ya panda na vuna.
Ikiwa kwa mfano, tunapatikana kwenye masafa moja ya utoaji na upokeaji na mtu mmoja au wengi na ikiwa watu hao wanapokea ujumbe wetu mbaya, tunaongeza basi uovu ndani mwao. Wataanza kuurudilia mara na mara ujumbe mbaya huo na hatimaye, kufikia pengine kuenenda kwa hali ya uovu au isioruhusiwa. Kwa hiyo tutakuwa tumefungwa kwao na sehemu ya ujumbe wetu uliowasababisha kutenda matendo hayo.
Ndiyo sababu fanya angalisho !

Uovu huvuta uovu na yote huongezeana nguvu, vilevile jambo nzuri huvuta mema na vyote pamoja huongezeana nguvu. Kama vile inavyotoka kufafanuliwa, mambo yote, hakika yote, yanaturudilia, iwe jambo mbaya au jambo jema. Kila mtu huamua mwenyewe jinsi ya kuongoza maisha yake. Tunaweza kugeukia Mtoaji wa ulimwenguni pote, yaani Mungu ndani mwetu, na kupata suluhisho mzuri katika hali tofauti tunayoyapitia mchana, tunaweza kurekebisha hali zetu mbovu na kupokea hivyo kila siku nguvu halisi, au tena tunaweza kuacha matukio yafuate mwelekeo mbaya.
Mtu anayedumisha hisia, mawazo au maneno mabaya, anapahswa kutarajia kupokea mabaya. Hakika tunaweza kusema kwamba kila mtu ni chanzo cha raha yake mwenyewe.

Mungu hakututolea Amri zake bure kupitia Musa. Si kwa bure ndio Mwana wa Mungu aliishi pamoja nasi kama Yesu wa Nazareti kwa kutuletea habari njema ya Uzima, iliyo neno la uzima katika Mafundisho yake mlimani.

Amri za Mungu na mafundisho ya Yesu wa Nazareti vinatuhimiza kumgeukia Mtoaji wa ulimwenguni pote, Roho huru milele, kwa kuwa Roho huru peke yake, Mungu wa kweli, ndiye anayeweza kutusaidia kutambua kile ambacho kila mmoja wetu angeweza kujifunza ili afikie maadili halisi, iliyo ya msingi. Amri kumi na Mafundisho ya Yesu mlimani vinatufundisha, kwa mfano, mwenendo gani tunaweza kuwa nao mbele ya jirani yetu, vinatufundisha tena namna ya kupata suluhisho nzuri, suluhisho zenye mafanikio kwa matukio tofauti ya siku.



Ndani ya Mtoaji mtukufu wa ulimwenguni pote, yaani Mungu, mna pia maisha ya wanyama na mimea; dunia nzima inajaa ujumbe wake.
« Usikate tumaini, stahimili ! », ina maana pia kwamba katika hali zote ni vema kwanza kubaki kimya kwa ajili ya kumgeuikia Mtoaji wa ulimwenguni pote, Mungu, ambaye peke yake ndiye msaada wa kweli.

Mungu, Roho wa Baba yetu wa Mbinguni, anayejua mambo yote, anataka kutuunga mkono na kutusaidia, lakini, mara nyingi kwa namna tofauti na mahitaji yetu. Yeye, Roho mtukufu, anajua kabla ya yote yaliyo bora kwa nafsi, baadaye anaangalia yale yaliyo bora kwa mwanadamu.

Yule anayehitaji kujifunza kufikia maadili ya kiwango cha juu na kupangilia upya uwezo wake wa utoaji juu ya mazuri, juu ya yale yanayoambatana na mapenzi ya Mungu, anaweza pia kuchunguza kile kinachojitokeza ndani ya ubongo wake. Kwani yule anayekasirika wakati anapopoteza utulivu wake, ana-

weza kuwa na uhakika kwamba ujumbe fulani umejitokeza mwilini mwake. Hayo ni dalili kwamba tungepashwa kuchambua hisia na mawazo yetu kwa ajili ya kugundua uzito wa ujumbe tuliotolewa. Tukikusudia kuipa maisha yetu mwelekeo mpya, ni vema, kupangilia upya namna yetu ya kufikiri.

Wakati wa kila mwelekeo mpya, ambao unasababisha bila shaka mpangilio mpya, tungepashwa kwanza kugeukia upande wa Mtoaji wa ulimwenguni pote, Mungu. Kwa msaada wa Aliye juu sana, mtu anayetegemea maadili ya kiwango cha juu, hutambua upesi kwamba wakati ujumbe mbaya unataka kuingia katika hisia zake, ujumbe mwengine huu unamuhimiza:

« Usikate tumaini, vumilia ! Mimi, upendo wa ulimwenguni pote na hekima, niko kando yako. Tambua yale unayotoa na rekebisha yale yaliyo ya uovu ».

Neno linalotoka ndani ya uzima halisi linasema:

« Geukia upande wa masafa ya utoaji wa juu sana kusudi upokee kupitia utajiri wa Mtoaji ambaye Niliye mimi, Mtoaji wa ulimwenguni pote, Roho aliye kila mahali, Mungu ndani mwako ».

Tukitaka na tukitumia vema mchana kwa manufaa yetu kwa lengo la kujifunza kupitia kila jambo linalotufikia, ili tupatie maisha yetu mwelekeo mpya, kila mmoja wetu atatambua jinsi wakati unavyopita kwamba ana nia ya kuongozwa na chemchem ya milele inayomuunga nkono, inayotoa wema, heshima na msaada. Hayo yanamaanishaa vilevile kuwa na nidhamu siku baada ya siku na kutumia vema nguvu zako ili kufikia nguvu za kiwango cha juu yaani nguvu halisi, iliyo pia na ujumbe mzuri.

Turudilie: hata mwanadamu awe na mwenendo mzuri au mbaya kupitia mawazo, hisia, maneno na matendo yake, hakika ni yeye mwenyewe ndiye sababu ya yale yanayompata.
Ndiyo maana tumepewa shauri hili linalorudiliwa: « Usikate tamaa, vumilia » ili tujipange

sawa sawa kila siku kwa maana akili halisi ya ulimwenguni pote, Mungu, anaishi ndani mwako !

Tunadhani au tunasema upesi sana kwamba jirani yetu ndiye chanzo cha shida fulani ambayo haikutatuliwa au wa hali mbaya hii au ile. Ni mara haba ndio tunatafuta kutambua sehemu yetu katika hali mbovu. Ijapokuwa, tukichukua fursa na kufikiri kabla ya kusema, tutatambua upesi kwamba sisi wenyewe tuna sehemu ya wajibu katika kile kinachopashwa kutatuliwa.
Shauri hili « Usikate tamaa, stahimili ! » linaweza kutusaidia hatua kwa hatua kuwa waangalifu na wenye kujitambua wenyewe, katika dhamiri tendaji: sikate tumaini kwa sababu Mtoaji wa ulimwenguni pote, Mungu, upendo, anatia ndani mwangu wema na msaada, na kwamba ninaweza kupokea neema hii kubwa ya ulimwenguni pote.

Inawezekanaje kuwasiliana na nguvu nzuri, na kuzipokea ? Kwa kufikia vema hayo, njia moja peke yake ni kupanga tena upya masa-

fa ya utoaji wetu. Mpango mzuri huo mpya ni kujaribu kutimiza Amri kumi za Mungu na Mafundisho ya Yesu mlimani.

Kwa ajili ya kupatia maisha yetu mwelekeo mpya, hatungepashwa kurizika tu na kusoma Amri kumi za Mungu na Mafundisho ya Yesu mlimani kama vile tusomavyo kitabu au kupekua kurasa zake. Kwa kuchukua mwelekeo mpya, inatubidi kuelewa maana ya ndani ya amri za Mungu na ya mafundisho ya Yesu mlimani na pamoja na hayo kuvilinganisha na mawazo, maneno na matendo yetu. Ni njia moja peke yake ya kuwa na dhamiri ya yale tunayowaza kila wakati na ni hivyo ndivyo tunaweza rekebisha uwezo wetu wa utoaji.

Watu wengi hawafikirii sana juu ya yale wanayotoa siku kwa siku hata pia juu ya yale wanayoyapokea. Dunia ya leo inafanana na pipa la, na baruti ndani mwake, baruti ndiyo uwezo wa ujeuri wa wanadamu wengi. Na kama uwezo wa utoaji wa wanadamu unajaa ugomvi, nini basi ambayo watakayopokea nao isipokuwa ugomvi ? Hayo yatafikia wapi

ikiwa tunaendelea kutoa hisia kama na hizo ? Kimatendo, kudumu kwa hali hiyo kunaweza kusababisha magombano, wizi, vita, uaji wa hiari na mauaji. Basi, fikra mbovu hazikosi madhara.

Tunaelewa leo kwamba mawazo pia ni nguvu ambazo tunatoa na ambazo hatimaye hutu-rudilia. Tafadhali, msiseme kwa haraka:
« Mawazo yangu ni mazuri kwa sehemu ku-bwa ». Tusijidanganye ! Mara na mara hali ya nje hudanganya.

Tunatambua hayo mara tu tunapochunguza yaliyomo ndani ya fikra zetu, tukichunguza mambo tunayoyafikiria. Tunadharau mara nyingi jambo hilo na kusema eti ni hisia tu, au tamaa tu, inabidi tuwe na dhamiri ya kwam-ba nayo ni nguvu pia. Jinsi wakati unavyopita, mtu hugeuka kile anachokitoa (yaani hufana-nishwa na mawazo, hisia, matendo na ma-neno yake). Hiyo huwa sasa tabia yake, na ambayo katika hali moja ni vigumu kuificha. Ndiyo maana, kila mmoja wetu anahusika na swali hili: je ! nakata tumaini au la ? Usalama

mmoja na wa kweli, katika hali zote ni, Mtoaji wa ulimwenguni pote, akili ya ulimwenguni pote, anayeitwa Mungu katika nchi za magharibi.

Kama jinsi tumetoka kusoma tayari, kila mmoja wetu ana uamzi juu ya maisha yake, kwa maana kila mmoja ni mhusika wa mawazo yake, maneno na matendo yake. Ndiyo maana shauri hili linalorudiliwa bila kukoma: mgeukieni Mtoaji wa ulimwenguni pote, Mungu, na mpangilieni maisha yenu kwa kumtegemea, kufuatana na Amri kumi ambazo alitutolea kupitia Musa, na Mafundisho ya Yesu mlimani.

Wamoja wamekwisha kutambua kwamba haiwezekani kupokea msaada toka nje. Siku moja au nyingine, kila mtu atatambua kwamba msaada wa kweli unaotutolea faraja na kutuunga mkono unatoka kwa Mungu peke yake, Mtoaji wa ulimwenguni pote wa upendo wa Mungu na wa jirani, anayetoa ndani mwetu, ndani ya nafsi yetu, ndani ya kila mwanadamu.

Fikirieni kwa busara dini zinazotangaza kwa uongo kuwa Mungu, wa milele, analipiza kisasi na kuadhibu. Kwa kweli, mnajiadhibu wenyewe kupitia hali mbaya mnazotoa na kupokea mara tena, na zinazowasukuma kufanya uovu, kutenda mkipingana na Mungu.

Tuwe na dhamiri ya kwamba Mtoaji wa kweli na wa milele ni wema, upendo, rehema, na msaada katika hali yote. Yeye ni Roho huru na wa milele anayetoa ndani ya nafsi ya kila mmoja. Anayemgeukia Mungu na kuelekeza uwezo wake wa utoaji kwake, ndiye anayepokea kupitia chemchem ya uzima safi wa milele wa Roho huru.

Wamoja wanaweza kujiswali ni sehemu gani panapopatikana kituo cha utoaji na cha mapokezi ndani ya mtu. Kituo hicho ni ubongo. Ni ubongoni ndimo tunarekodi yaliyomo katika hisi, hisia zetu, mawazo, maneno na matendo yetu.Tunajaza ubongo wetu na mambo hayo yaliyo rekodiwa.
Mambo yaliyorekodiwa ubongoni mwetu hufanana kwa sehemu ndogo na progamu

za televisheni kwani tunarekodi mambo kwa sehemu kubwa kama picha. Hayo yaonesha urefu wa mawimbi yetu. Ubongo wetu hutolea mwili mpangilio wake, na kupitia mwili, inautowa kwa nafsi yetu. Hivyo ndivyo tabia na mwenendo wetu hujidumisha, na kujionesha mwilini kwetu. Hayo ndiyo yaonesha hali yetu ya nje.

Kwa mfano, mtu akifa leo, nafsi, iliyotoka mwilini mwake, hubaki hata hivyo nafsi hiyo hiyo. Baada ya kifo cha mwili, nafsi yanabaki yale yale kama jinsi ilivyokuwa mwilini. Hata kama mtu huyo alikuwa mtu wa hali duni au hata kama alipewa vyeo na ana utajiri, mara moja baada ya kifo cha mwili, mtu na nafsi yake hubaki bila cheo wala mali. Nafsi peke ndiyo hudumu bali si kitu kingine. Ndiyo maana kila siku ya maisha yetu duniani ni ya muhimu. Kwani mti hubaki ukilala jinsi ulivyoanguka ! Kila wakati ni muafaka kwani kila wakati mtu hutoa na kupokea.



Tukumbushe mara tena, kwa lengo la kuelewa vema, jambo muhimu kwa kila mmoja wetu: Jinsi tunavyotoa sana mipangilio zinazofana-na ndivyo nguvu za kufanana zinachukua uwezo ubongoni mwetu na mwilini mwetu. Nafsi yetu, mwili ulio na umbo la kiroho, ina-irekodi vilevile.

Tuyarudilie: Mipangilio yote ambayo ilikuwa bado ndani mwetu asubuhi, yanaendelea kui-shi hata kama mwili wetu unakufa kwa gafla mchana huo. Nafsi inabaki ile ile kama waka-ti ilipokuwa mwilini. Mti uliokatwa unaende-lea kubaki wa aina ile ile ya kabla ya mti huo kukatwa. Haifai tuamini kwamba siku moja, wakati tutakufa tutakuwa watu wengine. Naf-si haiwezi kwenda na kitu cha kimwili. Mzigo wake mmoja ni mipango au mambo ambayo mtu aliitwika.

Tulipashwa mara na mara kujiswali: mimi ni nani leo ? Nitakua nani kesho ? Watu wengi huamini kwamba hakuna siku zijazo kwao na kwamba wanaendelea kuishi kupitia jeni za wana wao na za wajukuu wao. Ni vema tuji-

swali kama jeni, ambayo ni mata hufanya kazi kubwa kama na hiyo.

Kwani ingekuwa kinyume cha haki kama watoto na wajukuu wetu wangeweza kurithi mipangilio yetu na kurekebisha mambo mabaya ambayo tulijitwika sisi wenyewe.

Baada ya kifo cha mwili wetu, tunaendelea kuishi kama nafsi, na kama ilivyosemeka hapo awali, mti hubaki ukilala jinsi ulivyoanguka. Ndiyo maana tungepashwa kutumia vema siku zetu kwa kujitambua na kwa kutambua kesho tutakuwa nani, kwa sababu nani anayejua wakati mti utaanguka ?



« Usikate tumaini, vumilia ! » ina maana ya kugeukia kila siku Mtoaji wa ulimwenguni pote, Mungu, aliyetutolea Amri kupitia Musa na Mafundisho ya Mlimani kupitia Yesu.

Usiache kamwe ! Hata katika hali ngumu sana, sali na uombe msaada !
Amini nguvu yenye uwezo wa ajabu inayotaka kukusaidia !

Ikiwa leo inawezekana hujahisi kupata msaada, yawezekana hata kesho pia, siku moja au nyingine nuru ya tumaini, mwanga ndogo, utakujia na utangaa ndani mwako. Ni Roho anayekuita. Ni upendo wa Mungu ndiyo unakugusa. Ndani ya nuru hiyo ndogo mnajidokeza tumaini na imani.

Usizime mwenge huo mdogo. Usikate tamaa, vumilia ! Sali na kuomba ! Usikate tumaini ! Ndani mwako mna uzima wa milele, na uzima wa milele ni upendo, wema, msaada na uungaji mkono. Uzima wa milele upo wakati wote. Ni Mungu. Mmoja wa ulimwenguni pote.

Usibaki katika maeneo ya hatari ya hali za kiutu ! Amua kuwa na ustahimilifu, katika dhamiri kwamba mahali fulani panajitokeza nuru ndogo yenye kutoa tumaini, uamanifu, msaada na uungaji mkono.

Chunga maneno haya ndani mwako: Usikate tumaini, vumilia ! Usikate tumaini, hata kama unapitia siku ngumu, saa za uzuni, zakukatisha tumaini. Katika sala, amsha uaminifu, amsha mwanga huo ndogo uliofichama.

Amini nguvu iliyo na utukufu wa ajabu ! Mtolee sala zako ! Ikiwa unahitaji, chukua Amri kumi za Mungu na Mafundisho ya Yesu mlimani na uisome.

Hebu, acha Amri kumi za Mungu na Mafundisho ya Yesu mlimani vitende kazi ndani mwako na mara moja utasikia sauti moja inayosema nawe.
Shikilia hayo. Usitupilie mafundisho hayo ! Mafundisho hayo ni mwanga mdogo au mwenge mdogo unaoleta msaada na uungaji mkono, kiasi kwamba, kwa msaada wa nguvu

za Kristo wa Mungu, inakuwezesha kuchambua mwenendo wako mbaya na kutambua sehemu yako katika hali za shida na zisizo na tumaini. Na punde si punde utatambua kwamba kauli hii « Usikate tumaini, vumilia ! » ni zawadi ya thamani kubwa toka Mbinguni.



Free Brochures / Brochures gratuites



Message of Truth

- Find God. Where? How?
- Reincarnation – Life's Gift of Grace
- Don't Let Go!
- Comfort in Need and Suffering
- A fulfilled Life Into Old Age

Le message de la vérité

- Dieu en nous
- Des perles de vie
- Vous n'êtes pas seul
- Vous vivez éternellement, la mort n'existe pas
- Le Sermon sur la Montagne, la clé d'une vie intérieure riche

Kitabu katika lugha ya Kiswahili kinachotelewa bila malipo:

- Mungu ndani mwetu



Info at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05



Gabriele Publishing
The Word

Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany

www.gabriele-publishing.com